

Miuhtasari ya Mkutano



Msaada kutoka kwa Roho Mtakatifu

Rais Eyring alisema kwamba yeye anahisi kutiwa moyo wakati anaposoma hadithi ya Nefi akiyachukua mabamba ya shaba kutoka kwa Labani. Nefi hakujuwa hasa cha kufanya, lakini yeye aliongozwa kila dakika na Roho Mtakatifu. Wakati Bwana anapotutaka tufanye jambo gumu, Roho Mtakatifu atatusaidia pia.



Hii inanifundisha:



Imani katika Yesu Kristo

Mzee Costa alishiriki hadithi ya wakati ambapo Yesu Kristo alituliza dhoruba. Sisi sote tunazo dhoruba, au changamoto, katika maisha ambazo ni ngumu. Lakini kamwe hatutakabiliana nazo peke yetu. Kuwa na imani katika Yesu Kristo kunatupatia sisi nguvu na amani tunayohitaji ili kukabiliana na dhoruba yo yote.



Hii inanifundisha:



Kumbuka Wewe U Nani

Mzee Stevenson alitulika sisi tusimame kila wakati tunapojiona wenyewe kwenye kioo na kusema, "Wee, hebu hitazame! Mimi ni wa kupendezza! Mimi ni mwana wa Mungu, Yeye ananijua! Yeye ananipenda!" Kufanya hivi kutatusaidia kukumbuka sisi ni kina nani kweli na jinsi gani Mungu na Roho Mtakatifu wanawenza kutusaidia.



Hii inanifundisha:



Kutembea katika Njia pamoja Naye

Rais Freeman alisimulia hadithi kuhusu wakati yeye alipoenda kutembea kwenye njia maalum, licha ya kuwa alikuwa ameumia kiwiko chake cha mguu. Hangeweza kutembea kwenye njia ile peke yake, kwa hiyo mwongozaji wa njia ile alimsaidia. Kama vile mwongozaji wa Rais Freeman, Yesu Kristo atatusaidia katika changamoto yo yote kama tunajitahidi kushika maagano yetu.



Hii inanifundisha: